



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



## TUME YAKUTANA NA VYAMA VYA SIASA KUJADILI UWEKAJI WAZI WA DAFTARI LA AWALI NA UBORESHAJI WAKE KWA AWAMU YA PILI

**Dar es salaam, 23 Machi, 2020**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi leo imekutana na wadau wake wakuu (wawakilishi wa vyama vya siasa) ikiwa ni maandalizi ya zoezi la uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura na uboreshaji wa awamu ya pili wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji Rufaa (Mst) Semistocles Kaijage amewaambia wadau hao kwamba mazoezi hayo ambayo yataenda sambamba yanatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 17 April 2020. "Uboreshaji wa Daftari Awamu ya Pili ambao utaenda sambamba na Uwekaji wazi wa Daftari la Awali utafanyika katika "routes" tatu. Route ya kwanza inatarajiwa kuanza tarehe 17 Aprili, 2020," amesema Jaji Kaijage. Aliongeza kwamba katika Uhakiki wa taarifa za Wapiga Kura njia zifuatazo zitatumika; Wapiga Kura wenyewe kufika katika vituo walivyojiandikisha na kuhakiki taarifa zao; kwa kutumia mfumo wa *Voters' Interaction Systems (VIS)*, ambapo Mpiga kura kupitia simu yake ya kiganjani atapiga namba **\*152\*00#**; kwa kupitia Tovuti ya Tume ([www.nec.go.tz](http://www.nec.go.tz)) na kwa kupitia kituo cha Huduma kwa Wapiga Kura (*Call centre*) ambapo wananchi watapiga simu bure kupitia namba **0800782100**. Aidha, kuhusu ratiba kamili na maeneo yatakayoanza kutekeleza mazoezi hayo, Jaji Kaijage amesema Tume itatangaza baadae.

Katika hatua nyingine, Jaji Kaijage amesema uchambuzi wa taarifa za zoezi la Uboreshaji kwa Awamu ya Kwanza unaonesha kwamba, Wapiga Kura wapya walioandikishwa ni **7,043,247** sawa na asilimia **30.41** ya Wapiga Kura walioandikishwa mwaka 2015. Amesema kwamba idadi hii imezidi matarajio na

makadirio ya awali kwa asilimia **13.41**. "Wapiga Kura waliojitokeza kuboresha taarifa zao ni **3,225,778** sawa na asilimia **13.93** ya Wapiga Kura walioandikishwa mwaka 2015. Aidha, jumla ya Wapiga Kura **16,707** sawa na asilimia **0.07** ya Wapiga Kura walioandikishwa mwaka 2015, waliondolewa kwenye Daftari kwa sababu wamefariki na wengine kupoteza sifa," ameeleza Jaji Kaijage.

Jaji Kaijage amesema jumla ya Wapiga Kura waliopo katika Daftari la Awali kwa sasa ni **30,187,987**. Na akafafanua kwamba idadi hii inaweza kubadilika baada ya kukamilika kwa zoezi la uhakiki na uchakataji wa taarifa za Wapiga Kura endapo watabainika waliojiandikisha zaidi ya mara moja.

Imetolewa na:

**Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga Kura  
Mkurugenzi wa Uchaguzi**